

**OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA BUTIAMA  
SHULE YA SEKONDARI MASABA  
S.L.P 343 BUTIAMA**

**MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MASABA KIDATO CHA KWANZA 2021**

**JINA LA MWANAFUNZI** \_\_\_\_\_

Ninafurahia kukutarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza 2020 katika shule ya Sekondari **MASABA** ambayo ni shule ya kutwa. Shule itafunguliwa tarehe 11/01/2021.

Unatakiwa kufika shule bila **KUKOSA tarehe 11/01/2021. ukiambatana** na Mzazi AU MLEZI WAKO. Masomo yataanza mara moja tarehe tajwa. KWA VYOVYOTE VILE HUTAKIWI KUKOSA SHULE SIKU YA KUFUNGUA SHULE. KWA WALE WENYE SABABU MAALUMU ZA KUFANYA KUTORIPOTI SHULENI SIKU YA KUFUNGUA, MWISHO WA KURIPOTI NI **11/01/2021**. BAADA YA TAREHE TAJWA WALE AMBAO WATAKUWA BADO HAWAJARIPOTI SHULENI, HATUA KALI ZA KISHERIA ZITACHUKULIWA DHIDI YA WAZAZI AU WALEZI WAO.

**MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

**1.0 SARE YA SHULE**

- SURUALI MBILI ZA RANGI YA KAKI na NYEUSI (kwa wavulana) zilizoshonwa kwa unadhifu, senye malinda mawili na mifuko ya mbele ya mshazari na mfuko mmoja wa nyumA
- 1. SKETI MBILI RANGI KAKI Na NYEUSI zenye marinda (kwa wasichana) ndefu zinazogusa visigino zilizo za heshima kusitiri mwili wa mtoto wa kike.
- Viatu nyeusi vya ngozi vya kufunga na kamba visivyo na visigino virefu (wavulana na wasichana).
- Shati mbili nyeupe mikono mifupi (wavulana na wasichana).
- Soksi nyeusi ndefu jozi mbili (wavulana)
- Soksi nyeupe ndefu jozi mbili (wasichana)
- Tai ndefu ya rangi ya kaki na nyeusi ) wavulana na wasichana.
- Sweta rangi ya BLUE mikono mirefu lenye shingo la V (wavulana na wasichana).
- Mkanda mweusi kwa wavulana.
- T- shirt rangi ya kijani (Jani la Mgomba) yenye nembo ya shule.

**2.0 VIFAA VINGINE**

- Daftrai zisizopungua 12 (unashauriwa kununua Counter books quire mbili kwa urahisi wa matumizi ya uhifadhi wa notice za mwanafunzi kwa muda mrefu.
- Mathematical set 1.

**3.0 MATIBABU, CHAKULA NA UJI KWA MWANAFUNZI WA KUTWA**

Shule haitoi huduma ya matibabu, chakula wala uji kwa mwanafunzi hivyo ni jukumu la mzazi au mlezi wa mwanafunzi husika.

#### **4.0 MAMBO MENGINE MUHIMU**

#### **SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE SEKONDARI MASABA .**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na 10 ya mwaka 1995. Aidha shule inazingatia miongozo yoyote inayotolewa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu yenyе dhamana ya elimu nchini na ofisi ya Rais TAMISEMI yenyе dhamana ya usimamizi na uendeshaji wa Elimu.

#### **UNATAKIWA KUZINGATIA MAMBO YA MSINGI YAFUATAYO:-**

- Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla.
- Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule.
- Kuwahi katika kila shughuli ya shule na nyingine utakazopangiwa.
- Kuвая sare ya shule muda wote uwapo/ kuwakilisha shule.
- Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
- Kutunza mali ya umma.

#### **MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE.**

- Wizi
- Usherati na ushoga
- Ubakaji
- Ulevi wa matumizi ya madawa ya kulevyा
- Kupigana na kupiga
- Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
- Kuoa au kuolewa
- Kuwa mjamzito au kusababisha ujauzito.
- Kutoa mimba.
- Kugoma, kuchochea, kuongoza na kushiriki katika mgomo na kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
- Kukataa ashabu kwa makusudi.
- Kuwa na simu ya mkononi.

Tafadhali ufikapo shulen i fika na Medical Examination form (imeambatanishwa ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya serikali. Fomu hii itakakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara unaporipoti shulen.

#### **KARIBU SANA KATIKA SHULE SEKONDARI MASABA**

MAHENDE M. MABURUGI

**MKUU WA SHULE YA SEKONDARI MASABA**

0766093752

**SHULE YA SEKONDARI MASABA  
AHADI/KIAPO CHA MZAZI NA MWANAFUNZI**

**SEHEMU A: (IJAZWE NA MWANAFUNZI MWENYEWE)**

Mimi ..... nakubali bila kushurutishwa kuchukua nafasi niliyopewa na taifa kujiunga ba kidato cha kwanza katika shule ya Sekondari MASABA Naahidi kutii sheria na taratibu zote za shule na kwamba nitajitahidi kujiendeleza kielimu kadri ya uwezo wangu chini ya uongozi wa walezi wangu hapa shulenii. Ninatambua kabisa kutenda kosa ni kibyume kabisa na sheria na taratibu hizi naomba uongozi wa shule unichukulie hatua kali za kinidhamu. Naahidi kuwa nitahudhuria shulenii muda wote bila kukosa kipindi hata kimoja

**EE MUNGU NISAIDIE.**

Tarehe ..... Sahihi.....

**SEHEMU B: (IJAZWE NA MZAZI/MLEZI MWENYEWE)**

Mimi .....(jina kamili) S.L.P..... ambaye nina uhusiano kamili na mwanafunzi .....  
Wa Sekondari MASABA ambapo kijana wangu amechaguliwa kujiunga na masomo ya elimu ya sekondari kidato cha kwanza.

Ninaahidi kumpatoa mahitaji yote yaliyoagizwa na shule na kwamba nitamuhimiza kijana wangu kufuata sheria na kanuni zote za shule kama ilivyoelekezwa.

Tarehe ..... Sahihi .....

**NB:** Fomu hii isijazwe na mtu yejote ikiwa wazazi wa mwanafunzi wapo hai, isipokuwa tu kama hawapo hai.

## **FOMU YA MAELEKEZO YA MWANAFUNZI NA MZAZI YA KUKUBALI NAFASI ALIYOPEWA.**

1. JINA KAMILI LA MWANAFUNZI \_\_\_\_\_
2. TAREHE YA KUZALIWA \_\_\_\_\_
3. SHULE ALIYOTOKA \_\_\_\_\_
4. MWANAFUNZI ANATOKA MTAAC WA / KIJIJI CHA \_\_\_\_\_
5. KATA YA \_\_\_\_\_ TARAFA YA \_\_\_\_\_
6. WILAYA YA \_\_\_\_\_ MKOA WA \_\_\_\_\_
7. JINA KAMILI LA MZAZI/ MLEZI \_\_\_\_\_
8. KAZI YA MZAZI/MLEZI \_\_\_\_\_
9. ANUANI YA MZAZI/ MLEZI \_\_\_\_\_ SIMU \_\_\_\_\_

- (i) Nimekubali nafasi niliyopewa na kuwa nitafuata sheria na taratibu zote za shule. Sheria zote na kanuni za shule nimezisoma na kuzielewa.
- (ii) Nitahakikisha kuwa nahudhuria shule siku zote za masomo.
- (iii) Nitahakikisha nasoma kwa bidii na maarifa. Sitashiriki katika vurugu za aina yoyote ile nikiwa mwanafunzi MASABA Sekondari. Nitadumisha nidhamu nzuri niwapo nje na ndani ya shuleni.
- (iv) Sitakuwa tayari kudhalilisha shule yangu.
- (v) Nitakubali kuchukuliwa hatua stahiki endapo nitakwenda kinyume na sheria za shule na za nchi.

.....  
**JINA LA MWANAFUNZI**

.....  
**TAREHE**

## **MEDICAL EXAMINATION**

**PARTY A:**

**TO THE MEDICAL OFFICER**

Please examine the person below as to his/ her physical and mental rightness for enrollment as a student. Examination should include the following categories.

.....  
i)

- (a) Eye - Sight .....
- (b) Hearing .....
- (c) Limbs .....
- (d) Speech .....
- (e) Venereal disease .....
- (f) Leprosy .....
- (g) Epilepsy .....

ii) Neuroses .....

iii) Other Serious Diseases .....

iv) Pregnancy if applicable .....

I have examined the above named person and consider that \*he/she\*  
Is /not physical and mental fit **SECONDARY EDUCATION.**

Date..... Name ..... Signature .....

Station ..... Designation .....